Kijarida Kuhusu

Hukumu

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

© LHRC

Septemba, 2013

Yaliyomo

SHUKURANI.....iv

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.....v

MAONO.....v

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI.....v

LENGO KUU.....vi

DIBAJI.....vii

1.0: UTANGULIZI.....1

1.1: Nini maana ya Hukumu.....1

1.1.1: Yaliyomo ndani ya Hukumu.....2

1.2: Tofauti iliyopo kati ya Hukumu, Amri na Uamuzi.....3

2.0: ATHARI ZA HUKUMU.....6

2.1: Kikaza Hukumu.....6

2.2: Yaliyomo kwenye Kukaza Hukumu...6

3.0 HITIMISHO.....8

SHUKURANI

Tunatoa shukurani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina tamani jamii yenye haki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika

vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

1.0: UTANGULIZI

Katika mashauri yote, yawe ya jinai au madai, mashauri hayo baada ya kufikishwa mahakamani na pande zote mbili kupewa fursa ya kusikilizwa mwishowe hakimu au jaji hutoa hukumu.

Lengo la kitini hiki ni kukuelimisha msomaji juu ya aina ya maamuzi mbali mbali yanayoweza kutolewa mahakamani. Sehemu ya maamuzi hayo hakimu anaweza kutoa Amri (*Order*) uamuzi (*Ruling*) au hukumu yenyewe (*Judgement*).

Baada ya kujadili kuhusu hukumu pia msomaji atapata fursa ya kufahamu maana na yaliyomo katika kikaza hukumu (decree).

1.1: Nini maana ya Hukumu

Hukumu ni uamuzi wa mwisho kabisa unaotolewa na mahakama juu ya suala linalobishaniwa baina ya mlalamikaji na mlalamikiwa. Uamuzi huo ndio unaotoa kauli ya mwisho na kutamka ni nani mwenye haki katika suala linalobishaniwa na ni nini wajibu wa yule aliyekosa ushindi.

1.1.1: Yaliyomo ndani ya Hukumu

Ili hukumu ikamilike inapaswa kuwa na mambo yafuatayo:-

(1) Jina la Mahakama inayosikiliza shauri.

(2) Majina ya mlalamikaji na mlalamikiwa au mshitaki na mshitakiwa.

(3) Maelezo ya lalamiko au shitaka.

(4) Hakimu anapaswa kutoa muhtasari wa mwenendo wa shauri linalobishaniwa mahakamani. Kwa ufupi hakimu ataeleza nani anamlalamikia nani? Hakimu atarejea kueleza kwa ufupi ushahidi uliotolewa na pande zote mbili katika shauri hilo.

(5) Hakimu ataeleza ni masuala gani ya msingi ambayo yanayobishaniwa.

(6) Baada ya hatua hizo hapo juu, ndipo hakimu hutoa uamuzi. Pamoja na hayo uamuzi ambao hakimu atatoa ni lazima uwe na sababu; yaani anapaswa kuonyesha ni sababu zipi zimemfanya afikie uamuzi huo.

(7) Jina la Jaji/Hakimu, sahihi yake, muhuri wa mahakama husika na tarehe ya uamuzi.

Katika kila linalobishaniwa lazima hakimu alitolee sababu ya uamuzi wake.

Mambo yaliyotajwa hapo juu ni muhimu sana kuzingatiwa. Iwapo moja wapo ya mambo hayo yatapuuziwa, basi hukumu hiyo itakuwa ni batili na upande wowote katika shauri hilo unaweza kukata rufaa kwenye mahakama ya juu zaidi au kuomba marejeo.

1.2: Tofauti iliyopo kati ya Hukumu, Amri na Uamuzi

Kama ilivyoainishwa hapo juu, hukumu ni uamuzi wa mwisho kabisa juu ya suala linalobishaniwa. Hata hivyo, kabla ya hukumu hiyo kutolewa, wakati shitaka linaendelea na iwapo kuna migogoro midogo midogo ilijitokeza, mmoja wa wahusika katika shitaka/shauri anaweza kupeleka mgogoro huo mdogo mahakamani na mahakama ikatolea uamuzi suala hilo wakati shitaka kuu (la awali) linaendelea. Hivyo basi, maamuzi yote yanayotolewa katika kutatua migogoro midogo midogo ndani ya shauri la msingi huitwa "uamuzi" (ruling). Hivyo basi, uamuzi ni ufumbuzi wa mgogoro mdogo uliojitokeza katika kesi kuu. Uamuzi si hukumu ya kesi kuu.

Mfano:

Uamuzi ni kama huu ufuatao, Mzee Chuma ni mfanyabiashara aishiye eneo la Kimara jijini Dar es Salaam. Mama Mashaka ni mkulima aishiye katika kijiji cha Boko- Bunju. Mzee Chuma ameingia katika kijiji cha Bunju na kuvamia shamba la Mama Mashaka na kuanza kuweka msingi wa kujenga nyumba. Mama Mashaka anapopata habari hizi anamfuata Mzee Chuma na kumfahamisha kwamba eneo hilo analojenga ni shamba lake. Mzee Chuma baada ya kupewa ujumbe huo anaamua kuupuuza na hivyo kuendelea na ujenzi kama kawaida.

Mama Mashaka anaamua kulipeleka suala hili mahakamani. Hata baada ya kesi kuanza Mzee Chuma anaendelea na ujenzi wake kama kawaida. Katika hali kama hii ya Mzee Chuma kuendelea na ujenzi ilihali kesi ipo mahakamani mwanasheria anamshauri Mama Mashaka kupeleka maombi ya kusimamisha ujenzi huo. Baada ya mahakama kuliangalia suala hilo iliona ni vyema kumsimamisha Mzee Chuma kuendelea na ujenzi huo.

Kitendo cha mahakama kumsimamisha Mzee Chuma kuendelea na ujenzi wa msingi wa nyumba ndicho kinachoitwa uamuzi. Uamuzi huu haukusimamisha shitaka ambalo liliendelea kuangalia ni nani mmiliki halali wa eneo linalobishaniwa.

Wakati mwingine hakimu huweza kutoa maagizo fulani ambayo mahakama inataka yatekelezwe mara moja; hii ndiyo inayofahamika kama amri (*Order*). Amri ni agizo au amuru la mahakama linaloupa nguvu za kisheria uamuzi.

Angalizo:

Izingatiwe kwamba, mara baada ya hukumu kufikia mwisho wa kusikiliza hoja juu ya suala linalobishaniwa mahakamani inapaswa kutoa hukumu. Hukumu hiyo inapaswa itolewe katika mahakama ya wazi ili kuwapa watu fursa ya kusikia uamuzi huo. Pamoja na hayo, hukumu hiyo lazima iandikwe na kutiwa saini ya hakimu aliyetoa hukumu hiyo au hakimu aliyeachiwa kutoa hukumu hiyo

iwapo hakimu aliyesikiliza mwanzo hakuweza kusikiliza mpaka mwisho kwa sababu zozote zisizozuilika.

2.0: ATHARI ZA HUKUMU

Hukumu inapotolewa humtangaza mshindi katika suala lililokuwa likibishaniwa. Baada ya mshindi kutangazwa mahakama inapaswa kutoa kikaza hukumu (Decree) ili kuipa nguvu hukumu hiyo na kumuwezesha mshindi matunda yanayotokana na hukumu hiyo.

2.1: Kikaza Hukumu

Kikaza Hukumu ni nini?

Ni amri inayotolewa na mahakama baada ya hukumu kutolewa ili kuitilia nguvu hukumu aliyopewa mshindi. Kikaza hukumu ni amri tekelezi.

2.2: Yaliyomo kwenye Kikaza Hukumu

Mambo yafuatayo ni lazima yawepo kwenye nakala yenye amri ya kikaza hukumu:-

(1) Kikaza hukumu lazima kiwiane na hukumu iliyotolewa.

(2) Lazima kionyeshe nambari ya shitaka husika.

(3) Lazima kionyeshe majina ya utambulisho wa wahusika kwenye shitaka hilo.

(4) Lazima kionyeshe maelezo ya mdai/dai.

(5) Lazima kionyeshe ni nafuu gani mahakama imemzawadia mshindi au na nafuu nyingine yoyote iliyotolewa na mahakama.

(6) Lazima kiwe na tarehe moja sawa na hukumu.

3.0 HITIMISHO

Katika kitini hiki tumeweza kujifunza nini maana ya hukumu, tofauti zilizopo kati ya uamuzi, amri na hukumu yenyewe. Pia mambo yanayopaswa kuwemo ndani ya hukumu. Imesisitiziwa kwamba ni lazima hukumu iwepo kwenye maandishi, isomwe kwenye mahakama ya wazi na iwekwe saini ya hakimu aliyetoa uamuzi. Tumejifunza pia juu ya kikaza hukumu na mambo yanayopaswa kuwemo ndani ya kikaza hukumu.

Inatupasa kufahamu kwamba, mara baada ya hukumu kutolewa, mtu yeyote asiyeridhika na hukumu iliyotolewa, sheria inampa nafasi ya kukata rufaa kwenye mahakama ya juu. Ili kukata rufaa, mrufani anapaswa kuandika barua kwenye mahakama iliyotoa maamuzi ili kuomba nakala ya hukumu/uamuzi na mwenendo wa shitaka/kesi, vitu hivi ndivyo vitakavyomsaidia mwanasheria, mrufani mwenyewe au mshauri mwingine yeyote yule kubaini suala la kisheria ambalo mahakama haikulizingatia na kutoa haki kinzani. Ni muhimu mrufani akazingatia muda uliowekwa kisheria katika kupeleka rufaa yake kwenye mahakama ya juu ili rufaa hiyo isipitwe na wakati, na sababu rufaa za lazima ziambatane na nakala ya hukumu na amri.